# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1002

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-737-1

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI
# ELIMU YA SEKONDARI
# KIDATO CHA I – IV
# 2023

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2023

ISBN 978-9987-09-737-1

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kudurufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo


Orodha ya Majedwali ..... iv
Vifupisho ..... v
Shukurani ..... vi
1.0 Utangulizi ..... 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ..... 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV ..... 2
4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV ..... 3
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ..... 3
6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 5
    6.1 Mwalimu ..... 5
    6.2 Mwanafunzi ..... 6
    6.3 Mzazi ..... 7
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 7
8.0 Zana/Vifaa vya Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 8
9.0 Upimaji ..... 8
10.0 Idadi ya Vipindi ..... 9
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 9
Kidato cha I ..... 10
Kidato cha II ..... 23
Kidato cha III ..... 32
Kidato cha IV ..... 39
Babliografia ..... 48

# Orodha ya Majedwali


Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Kidato cha I – IV ........ 4

Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa Upimaji Endelevu ........ 9

Jedwali Na. 3: Maudhui ya Kidato cha I ........ 10

Jedwali Na. 4: Maudhui ya Kidato cha II ........ 23

Jedwali Na. 5: Maudhui ya Kidato cha III ........ 32

Jedwali Na. 6: Maudhui ya Kidato cha IV ........ 41

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| EAC | *East African Community* |
| LAT | Lugha ya Alama Tanzania |
| SADC | *Southern Africa Development Community* |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |

## Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za Serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa Muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala wa TET. Vilevile, TET inaishukuru kwa dhati Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Awali, Msingi, Sekondari, na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya Muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la maboresho ya mitaala ya mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa Muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Historia ya Tanzania na Maadili ni moja kati ya masomo ya lazima katika ngazi ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV kwa wanafunzi walioko katika Mkondo wa Elimu ya Jumla na Amali. Somo hili linafundishwa kwa lugha ya Kiswahili ili kujenga na kuendeleza mila, desturi na utamaduni wa Mtanzania. Vilevile, somo hili limelenga kumjenga Mtanzania mzalendo na mwajibikaji anayefahamu historia, desturi, mila na maadili ya Tanzania. Baadhi ya malengo ya somo hili ni kujenga maadili, kukuza utaifa na uzalendo pamoja na kulinda masilahi ya nchi na ya Taifa. Inatarajiwa kuwa somo hili litamwezesha mhitimu kuishi kwa kufuata misingi ya kuthamini kazi, uwajibikaji, utu, uadilifu, umoja, uzalendo, upendo na kuthamini rasilimali za Taifa.

Aidha, Muhtasari huu umeandaliwa ili kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muhtasari unatafsiri umahiri uliobainishwa kwenye Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV wa Mwaka 2023. Muhtasari huu ni mwendelezo wa muhtasari wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili wa Elimu ya Msingi Darasa la III – VI. Katika ngazi ya sekondari, Muhtasari huu umejikita katika ujenzi wa umahiri utakaomwezesha mwanafunzi kufahamu na kuilinda historia, urithi na maadili ya Taifa. Vilevile, umahiri utamwezesha mwanafunzi kumudu historia ya jamii za Kitanzania katika nyakati mbalimbali kabla na baada ya uhuru, kutathmini ujenzi wa Taifa na maadili wakati wa Azimio la Arusha na wakati wa uliberali na pia kumudu muundo na kazi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi na maendeleo endelevu ya Taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingiri; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV

Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV ni:

(a) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi na mwelekeo alioupata katika hatua ya elimu ya msingi;

(b) Kulinda mila na desturi, umoja wa kitaifa, Tunu za Taifa, demokrasia, kuthamini haki za binadamu na za kiraia, wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo;

(c) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia na kiufundi;

(d) Kuimarisha mawasiliano kwa kutumia stadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha mguso, lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha moja nyingine ya kigeni;

(e) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia na utunzaji endelevu wa mazingira;

(f) Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake; na

(g) Kukuza utayari wa kujiendeleza na mafunzo ya elimu ya kati na ya juu.

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV

Umahiri wa jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV ni:

(a) Kutumia maarifa na stadi alizozipata katika ngazi ya elimu ya msingi kuimarisha na kupanua uelewa wa masomo ya jumla;

(b) Kuthamini uraia na Tunu za Taifa;

(c) Kuonesha kujiamini katika kujifunza nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia na ya kivitendo;

(d) Kutumia stadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha mguso, lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha moja nyingine ya kigeni kuwasiliana;

(e) Kutumia maarifa ya masuala mtambuka kuyamudu mazingira yanayomzunguka; na

(f) Kutumia ujuzi na stadi kumwezesha kujiajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha na mazingira yanayomzunguka.

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Muhtasari wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Sekondari Kidato cha I – IV una umahiri mkuu na umahiri mahususi kama inavyooneshwa katika Jedwali Nambari 1.

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Kidato cha I – IV*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kulinda historia, urithi na maadili ya Taifa | 1.1 Kuelezea chimbuko la jamii za Kitanzania na maadili yake<br>1.2 Kumudu maarifa na ujuzi wa maadili na urithi wa jamii za Kitanzania<br>1.3 Kutumia maarifa na ujuzi wa historia na urithi kubuni fursa mbalimbali zilizopo katika jamii za Kitanzania<br>1.4 Kubaini fursa mbalimbali za kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa kitaifa |
| 2.0 Kumudu historia ya jamii za Kitanzania na maadili yake kabla ya ukoloni | 2.1 Kuchambua mifumo ya kijamii (elimu, afya, utamaduni, uchumi) iliyokuza na kuendeleza maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni<br>2.2 Kuchambua mifumo iliyokuza na kuendeleza uchumi na siasa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni<br>2.3 Kutathmini vichocheo vya mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni |
| 3.0 Kumudu historia ya Tanzania na maadili wakati wa ukoloni, 1890 – 1960 | 3.1 Kutumia maarifa na ujuzi wa chimbuko na ukuaji wa mfumo wa ukoloni kuelewa uhusiano wa kihistoria kati ya Tanzania na mataifa yaliyoitawala<br>3.2 Kutathimini athari za mfumo wa ukoloni kwenye maadili ya jamii za Kitanzania<br>3.3 Kuchambua jitihada za jamii za Kitanzania kupinga ukoloni na maadili ya kikoloni |
| 4.0 Kumudu historia ya ujenzi wa Taifa la Tanzania na maadili katika kipindi cha 1961 – 1966 | 4.1 Kuchambua mifumo ya uchumi, siasa, utamaduni, jamii na maadili iliyojengwa 1961 – 1966<br>4.2 Kumudu historia ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar<br>4.3 Kumudu historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar |

| | |
|---|---|
| 5.0 Kutathmini ujenzi wa Taifa na maadili wakati wa Azimio la Arusha, 1967 – 1985 | 5.1 Kuchambua chimbuko la Azimio la Arusha na matokeo yake kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kimaadili<br>5.2 Kueleza nafasi ya Tanzania katika kujenga uhusiano wa kikanda |
| 6.0 Kutathmini historia ya Tanzania na maadili wakati wa uliberali, 1986 hadi sasa | 6.1 Kuchambua chimbuko la uliberali na utandawazi<br>6.2 Kuishi maadili mema ya Kitanzania wakati wa uliberali na utandawazi |
| 7.0 Kumudu muundo na kazi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 7.1 Kueleza muundo na kazi ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar<br>7.2 Kubaini muundo na kazi za serikali za mitaa |
| 8.0 Kumudu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 8.1 Kuchambua muundo wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania<br>8.2 Kuchambua misingi ya Katiba ya JMT<br>8.3 Kutumia maarifa ya Katiba ya JMT katika shughuli mbalimbali za jamii na za kimaadili |
| 9.0 Kufanya kazimradi ya historia ya Tanzania na maadili | 9.1 Kufanya kazimradi ya historia ya Tanzania na maadili |

## 6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi.

### 6.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

(a) Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika somo la Historia ya Tanzania na Maadili;

(b) Kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia zitakazomwezesha mwanafunzi:

   (i) Kujenga umahiri unohitajika katika Karne ya 21; na

   (ii) Kushiriki ipasavyo katika tendo zima la ujifunzaji kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai na uwezo wa mwanafunzi;

(c) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zile zitakazomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali;

(d) Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;

(e) Kutengeneza na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;

(f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo;

(g) Kuhakikisha kuwa tendo la ujifunzaji na ufundishaji linafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;

(h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;

(i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;

(j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;

(k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa mwanafunzi; na

(l) Kuchopeka masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 6.2 Mwanafunzi

Mwanafunzi anatarajiwa:

(a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;

(b) Kupata umahiri unaokusudiwa kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa;

(c) Kushirikiana na wenzake pamoja na mwalimu katika mchakato wa ujifunzaji; na

(d) Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo vitabu vya kiada, ziada na machapisho mengine kutoka katika maktaba mtandao.

### 6.3 Mzazi

Mzazi/mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;

(b) Pale inapowezekana, kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma;

(c) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji;

(d) Kufuatilia mwenendo wa kitabia wa mtoto;

(e) Kumpatia mtoto vifaa muhimu vinavyohitajika katika shughuli ya ujifunzaji;

(f) Kuhakikisha mtoto anapata mahitaji muhimu; na

(g) Kumfundisha mtoto juu ya umuhimu na thamani ya elimu pamoja na kumhimiza kujifunza na kufanya kazi kwa bidii.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili utazingatia ujenzi wa umahiri na utatakiwa kufanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji. Mwalimu atakuwa mwezeshaji na atatakiwa kutumia mbinu zinazomshirikisha mwanafunzi katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai, na uwezo wa mwanafunzi. Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinatakiwa kuwa shirikishi ili zimwezeshe mwanafunzi kufikiri, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali, kufanya majadiliano katika vikundi, utafiti na kazimradi na kushiriki katika kutoa mrejesho. Mbinu nyingine ni ziara za kimasomo, na kazi za vitendo kulingana na mazingira ya shule. Aidha, mwalimu anahimizwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa.

## 8.0 Zana/Vifaa vya Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinapaswa kukidhi na kuendana na mahitaji, umri, na uwezo wa mwanafunzi. Mwalimu anapaswa kuhakikisha mwanafunzi anapata nafasi ama ya kuona, kusikia au kushika zana. Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji zitapaswa zimsaidie mwanafunzi kuelewa kinachofundishwa. Mwalimu anashauriwa pia kufaragua na kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yanayomzungumka. Zana za ufundishaji na ujifunzaji zilizopendekezwa ni pamoja na kompyuta, printa, tableti, CD, matini zenye historia na maadili, manila, chatipindu, michoro, picha, kinasasauti, runinga, redio, vitu halisi, vitabu, ramani na nyaraka mbalimbali. Zana hizi zimependekezwa katika jedwali la maudhui katika safu ya zana/vifaa. Aidha, orodha ya vitabu na vifaa kwa ajili ya rejea itatolewa na TET.

## 9.0 Upimaji

Upimaji wa maendeleo ya ujifunzaji ni suala muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu anashauriwa kuwa na uwanja mpana wa uchaguzi wa mbinu na zana za upimaji wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili ili kupima umahiri wa mwanafunzi wa kulinda historia ya Tanzania, urithi na maadili ya Taifa, kumudu historia ya Tanzania na maadili katika vipindi

mbalimbali na kutathimini historia ya ujenzi wa Taifa wakati wa uhuru, Azimio la Arusha na uliberali. Njia za upimaji ziwe zile zinazopima nadharia na vitendo zikiwemo bunguabongo, orodhahakiki, majaribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi, kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi. Njia nyingine za upimaji zinaweza kuwa majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya mihula na mtihani wa mwisho.

Aidha, upimaji utahusisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na mahitaji ya mwanafunzi katika ujifunzaji. Hivyo, upimaji endelevu utachangia asilimia 30 ya upimaji wote na upimaji tamati wa kuhitimu Kidato cha IV utachangia asilimia 70. Mgawanyo wa upimaji endelevu umebainishwa katika Jedwali Nambari 2.

**Jedwali Na. 2:** *Mgawanyo wa Upimaji Endelevu*

| Na. | Aina ya upimaji | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| 1. | Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Sita | 6.0 |
| 2. | Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili | 5.0 |
| 3. | Mtihani wa muhula wa mwisho wa Kidato cha Tatu | 5.0 |
| 4. | Kazimradi itayofanyika mwishoni mwa Kidato cha Tatu | 7.0 |
| 5. | Mtihani wa utamilifu (mock) wa Kidato cha Nne | 7.0 |
| 6. | Mtihani wa kitaifa wa Kidato cha Nne | 70.0 |
| | **Jumla** | **100** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo Historia ya Tanzania na Maadili unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za ujifunzaji za mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi viwili (2) kwa wiki kwa Kidato cha I – IV.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui ya Muhtasari huu yanawasilishwa katika jedwali lenye safu wima saba ambazo ni; umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa, vigezo vya upimaji, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa, na idadi ya vipindi kama inavyooneshwa katika Majedwali Nambari 3 – 6.

## Kidato cha I

**Jedwali Na. 3:** *Maudhui ya Kidato cha I*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Kulinda historia ya Tanzania, urithi na maadili ya Taifa | 1.1 Kuelezea chimbuko la jamii za Kitanzania na maadili yake | (a) Kueleza asili ya jamii za Kitanzania (Wabantu, Wanilo, Wakushito, Wakichembe) | **Bunguabongo:** Ongoza wanafunzi kubungua bongo ili kubainisha jamii mbalimbali za Kitanzania<br>**Kualika mtaalamu:** Ongoza mtaalamu kutoa maelezo kwa wanafunzi juu ya asili za jamii mbalimbali za Kitanzania.<br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi kwenye vikundi vidogovidogo kujadili na kuandika muhtasari wa maelezo yaliyotolewa na mtaalamu na kuwasilisha darasani. | Asili ya jamii za Kitanzania zimeelezwa kwa usahihi | Matini zenye kuonesha asili ya jamii za Kitanzania<br>Ramani kuonesha mtawanyiko wa jamii za asili<br>Vitu halisi vilivyotumiwa na watu wa jamii za asili | 9 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kubaini shughuli mbalimbali za makundi ya asili ya jamii za Kitanzania | **Fikiri-andika-jozisha-shirikisha:** Ongoza wanafunzi kufikiri, kuandika, kukaa katika jozi na kujadili shughuli walizoandika, kisha wajadili katika vikundi ili kuorodhesha shughuli mbalimbali za makundi ya asili ya jamii za Kitanzania. **Majadiliano:** Ongoza majadiliano ya darasa kujadili shughuli mbalimbali za makundi ya asili ya jamii za Kitanzania. | Shughuli za makundi ya asili ya jamii za Kitanzania zimebainishwa | | |
| | | (c) Kueleza maadili ya jamii za asili ya Kitanzania | **Bunguabongo:** Ongoza wanafunzi kujibu maswali kuhusu maadili ya jamii mbalimbali za asili. | Maadili ya jamii za asili ya Kitanzania yameelezwa kwa ufasaha | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kisa mafunzo:** Ongoza wanafunzi kusoma visamafunzo katika vikundi vyao kwa kutumia maswali yaliyotolewa ili kufanya uchambuzi wa kina.<br>**Majadiliano:** Ongoza majadiliano darasani kwa wanafunzi kuwasilisha walichojadili katika vikundi vyao kuhusu maadili ya jamii za asili za Kitanzania. | | | |
| | 1.2 Kumudu maarifa na ujuzi wa maadili na urithi wa jamii za Kitanzania | (a) Kuchambua maadili na urithi wa jamii za Kitanzania | **Changanyakete:** Gawa visamafunzo mbalimbali kuhusu maadili na urithi wa jamii za Kitanzania kwenye makundi. | Maadili na urithi wa jamii za Kitanzania yamecha-mbuliwa kwa ufasaha | Ramani kuonesha maeneo yenye urithi wa Tanzania<br><br>Vitu halisi vilivyotumiwa na watu wa jamii za asili | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili na kuandika muhtasari wa walichojifunza. | | | |
| | | (b) Kueleza matendo ya msingi yanayokuza na kulinda maadili na urithi wa jamii za Kitanzania | **Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogovidogo, kujadili matendo ya msingi yanayokuza na kulinda maadili na urithi wa jamii za Kitanzania. | Matendo ya msingi yanayokuza na kulinda maadili na urithi wa jamii za Kitanzania yameelezwa kwa ufasaha | | |
| | 1.3 Kutumia maarifa na ujuzi wa historia na urithi kubuni fursa mbalimbali zilizopo katika jamii za Kitanzania | (a) Kubaini fursa mbalimbali zilizopo kwenye urithi wa jamii za Kitanzania | **Utafiti mdogo:** Ongoza wanafunzi katika vikundi vyao watembelee na kubaini fursa anuai zilizopo katika maeneo wanamoishi zenye urithi wa jamii za Kitanzanai. **Matembezi ya galari:** Ongoza wanafunzi kuziorodhesha, kubandika | Fursa mbalimbali zilizopo kwenye urithi wa jamii za Kitanzania zimebainishwa | Matini kuhusu fursa kwenye urithi wa jamii za Kitanzania<br><br>Ramani kuonesha maeneo yenye urithi wa Tanzania<br><br>Vitu halisi vilivyotumiwa na watu wa jamii za asili | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | kwenye kuta za darasa, kufanya matembezi na kuuliza maswali katika vikundi mbalimbali. | | | |
| | | (b) Kueleza namna fursa zilizopo kwenye urithi wa jamii za Kitanzania zinavyoweza kutumika kukuza uchumi binafsi na jamii | **Kisamafunzo:** Ongoza wanafunzi kujadili kisamafunzo na kutoa maoni yao kuhusu fursa za urithi na manufaa yake katika jamii za Kitanzania. **Mtaalamu mwalikwa:** Ongoza wanafunzi kumsikiliza na kuuliza maswali mtaalamu kuhusu namna ya kutumia fursa za urithi katika kukuza uchumi binafsi na jamii. | Fursa zilizopo kwenye urithi wa jamii za Kitanzania zinavyoweza kutumika kukuza uchumi binafsi na jamii zimeelezwa kwa ufasaha | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kueleza njia mbalimbali za kutunza urithi wa jamii za Kitanzania | **Fikiri -andika-jozisha -shirikisha:** Ongoza wanafunzi kufikiri, kuandika, kujozisha na kushirikishana katika vikundi kuelezea njia mbalimbali za kutunza urithi wa jamii inayowazunguka.<br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi kufanya majadiliano katika darasa kuelezea njia mbalimbali za kutunza urithi wa jamii za Kitanzania. | Njia mbalimbali za kutunza urithi wa jamii za Kitanzania zimeelezwa kwa ufasaha | | |
| | 1.4 Kubaini fursa mbalimbali za kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa kitaifa | (a) Kuainisha shughuli mbalimbali za kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa Taifa | **Utafiti mdogo:** Ongoza wanafunzi kutembelea maeneo mbalimbali yenye shughuli mbalimbali za kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa Taifa. | Shughuli mbalimbali za kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa Taifa zimeanishwa | Matini kuhusu fursa mbalimbali za kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa kitaifa<br>Picha kuonesha shughuli mbalimbali | 8 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Matembezi ya galari:** Ongoza wanafunzi kwenye vikundi vidogovidogo kijadili, kisha waelekeze wabandike matokeo ya utafiti wao na kurekebisha pale palipokuwa na upungufu. | | Ramani kuonesha maeneo yenye fursa mbalimbali | |
| | | (b) Kufafanua namna shughuli mbalimbali zinavyochangia kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa Taifa | **Mtaalamu mwalikwa:** Ongoza mtaalamu kufafanua shughuli mbalimbali zinavyochangia ushirikiano na uchumi wa Taifa. **Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi vidogovidogo kujadili kisha kuwasilisha kwenye darasa kwa majadiliano. | Shughuli mbalimbali zinavyochangia kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa Taifa zimefafanuliwa kwa ufasaha | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kumudu historia ya Tanzania na maadili kabla ya ukoloni | 2.1 Kuchambua mifumo ya kijamii (elimu, afya, utamaduni) iliyokuza na kuendeleza maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | (a) Kubaini mifumo ya kijamii ya Tanzania kabla ya ukoloni | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini kutoka katika sehemu mbalimbali kama maktaba na Intaneti na kuandika kwa ufupi kuhusu mifumo ya kijamii za Tanzania kabla ya ukoloni.<br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili na kuwasilisha darasani kwa majadiliano ya pamoja. | Mifumo ya kijamii za Tanzania kabla ya ukoloni imebainishwa | Picha kuonesha miundombinu ya elimu, afya na utamaduni kabla ya ukoloni<br>Ramani kuonesha mtawanyiko wa miundombinu elimu, afya na utamaduni kabla ya ukoloni<br>Vitu halisi vilivyotumika kabla ya ukoloni | 10 |
| | | (b) Kueleza mifumo ya kijamii ya Tanzania ilivyokuza maadili kabla ya ukoloni | **Mtaalamu mwalikwa:** Ongoza wanafunzi kusikiliza na kuuliza maswali mtaalamu mwalikwa kuhusu jinsi mifumo ya jamii za Tanzania ilivyokuza maadili kabla ya ukoloni. | Mifumo ya kijamii ya Tanzania ilivyokuza maadili kabla ya ukoloni imeelezwa kwa ufasaha | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Majadiliano:** Ongoza wanafunzi kujadili katika vikundi jinsi mifumo ya kijamii ya Kitanzania ilivyokuza maadili kabla ya ukoloni kisha kuwasilisha darasani kwa majadiliano zaidi. | | | |
| | 2.2 Kuchambua mifumo iliyokuza na kuendeleza uchumi na siasa katika jamiii za Kitanzania kabla ya ukoloni | (a) Kubaini mifumo ya kiuchumi na kisiasa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini kutoka katika vyanzo mbalimbali na kuandika maelezo kuhusu mifumo ya kiuchumi na kisiasa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.<br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili na kisha kuwasilisha darasani kwa majadiliano ya pamoja. | Mifumo ya kiuchumi na kisiasa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni imebainishwa | Matini kuhusu mifumo ya kiuchumi na kisiasa kabla ya ukoloni<br>Ramani kuonesha maeneo mbalimbali ya jamii za asili za Kitanzania | 15 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kueleza jinsi mifumo ya kisiasa na kiuchumi ilivyokuza na kuendeleza shughuli za kiuchumi na kisiasa kabla ya ukoloni | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini na kuandika maelezo kuhusu jinsi mifumo ya kisiasa na kiuchumi ilivyokuza na kuendeleza shughuli za kiuchumi na kisiasa kabla ya ukoloni.<br>**Majadiliano:** Ongoza majadiliano ya vikundi kuhusu jinsi mifumo ya kisiasa na kiuchumi ilivyokuza na kuendeleza shughuli za kiuchumi na kisiasa kabla ya ukoloni | Mifumo ya kisiasa na kiuchumi ilivyokuza na kuendeleza shughuli za kiuchumi na kisiasa kabla ya ukoloni imeelezwa kwa ufasaha | | |
| | | (c) Kufafanua uhusiano kati ya jamiii za Kitanzania na za Mashariki ya Kati, Mashariki | **Changanyakete:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kusoma matini kuhusu uhusiano wa jamii mmoja ya Kitanzania na jamii za Mashariki | Uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na za Mashariki ya Kati, Mashariki ya Mbali na Ulaya katika | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ya Mbali na Ulaya katika kuendeleza shughuli za kiuchumi na kisiasa kabla ya ukoloni | ya Kati au Mashariki ya Mbali au Ulaya.<br>Elekeza kila kikundi kutoa mwakilishi mmoja kwenda kikundi kingine kufundisha walichojifunza katika kundi lao. | kuendeleza shughuli za kiuchumi na kisiasa kabla ya ukoloni umefafanuliwa kwa ufasaha | | |
| | | (d) Kutathmini mchango wa mifumo ya kisiasa na kiuchumi katika kukuza maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | **Kisamafunzo:** Elekeza wanafunzi katika vikundi kusoma na kuchambua faida na hasara za mifumo ya kisiasa na kiuchumi katika kukuza maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.<br>**Majadiliano:** Ongoza vikundi kuwasilisha darasani kwa majadiliano ya pamoja. | Mchango wa mifumo ya kisiasa na kiuchumi katika kukuza maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni umetathminiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.3 Kutathmini vichocheo vya mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | (a) Kueleza hali ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini na kuandika maelezo kuhusu hali ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.<br>**Majadiliano:** Ongoza majadiliano ya vikundi kuhusu hali ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. | Hali ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni imeelezwa kwa ufasaha | Matini kuhusu vichocheo vya mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni<br>Picha ya bidhaa zilizozalishwa na jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni<br>Ramani kuonesha maeneo yaliyokuwa ya uzalishaji wa bidhaa kabla ya ukoloni | 8 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kubaini vichocheo vya mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | **Kisamafunzo:** Elekeza wanafunzi kusikiliza kisamafunzo kuhusu vichocheo vya mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika jamii mojawapo ya Kitanzania kabla ya ukoloni. | Vichocheo vya mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni vimebainishwa | | |
| | | | **Maswali na majibu:** Uliza maswali kuwezesha wanafunzi kuzungumzia jamii zingine za Kitanzania | | | |

## Kidato cha II

**Jedwali Na. 4:** *Maudhui ya Kidato cha II*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu historia ya Tanzania na maadili wakati wa ukoloni, 1890-1960 | 1.1 Kutumia maarifa na ujuzi wa chimbuko na ukuaji wa mfumo wa ukoloni kuelewa uhusiano wa kihistoria kati ya Tanzania na mataifa yaliyoitawala | (a) Kuchambua chimbuko la ukoloni | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini kutoka katika vyanzo mbalimbali na kuandika maelezo kuhusu chimbuko la ukoloni.<br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili chimbuko la ukoloni na kisha kuwasilisha darasani kwa majadiliano ya pamoja. | Chimbuko la ukoloni limechambuliwa kwa kina | Matini kuhusu chimbuko la mfumo wa ukoloni<br>Picha mbalimbali kuonesha wataala na shughuli za wakoloni | 18 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kubainisha mataifa yaliyoitawala Tanzania na mifumo yake ya kikoloni katika uchumi, utawala na utamaduni | **Majadiliano:** Kwa kutumia maarifa waliyopata katika shughuli iliyotangulia, ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili na kuandika kwa ufupi kuhusu mataifa yaliyoitawala Tanzania na mifumo yake ya kiuchumi, kiutawala na kiutamaduni. | Mataifa yaliyoitawala Tanzania na mifumo yake ya kikoloni katika uchumi, utawala na utamaduni yamebainishwa | | |
| | | (c) Kujadili mchango wa mifumo ya kikoloni katika uhusiano wa Tanzania na mataifa yaliyoitawala | **Fikiri-andika-jozisha-shirikisha:** Ongoza kila mwanafunzi kufikiri, kuandika, kumshirikisha mwezake na kujadili katika kikundi kuhusu mchango wa mifumo ya kikoloni katika uhusiano wa Tanzania na mataifa yaliyoitawala | Mifumo ya kikoloni katika uhusiano wa Tanzania na mataifa yaliyoitawala imejadiliwa kwa kina | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kutathmini athari za mfumo wa ukoloni kwenye maadili ya jamii za Kitanzania | (a) Kueleza hali ya maadili ya jamii za Kitanzania kipindi ukoloni unaingia | **Changanyakete:** Gawa wanafunzi katika vikundi na kila kikundi kisome matini kuhusu hali ya maadili ya jamii mojawapo ya Kitanzania kipindi ukoloni unaingia. Kisha kila kikundi kitoe mwakilishi kwenda kikundi kingine kufundisha walichojifunza katika kikundi chao. | Hali ya maadili ya jamii za Kitanzania kipindi ukoloni unaingia imeelezwa | Matini kuhusu athari za mfumo wa ukoloni kwenye maadili ya jamii za Kitanzania | 14 |
| | | (b) Kuchambua athari za mfumo wa ukoloni katika maadili ya jamii za Kitanzania | **Utafiti mdogo:** Elekeza kila mwanafunzi kusoma matini kutoka katika vyanzo mbalimbali na kuandika maelezo kuhusu athari za mfumo wa ukoloni katika maadili ya jamii za Kitanzania. | Athari za mfumo wa ukoloni katika maadili ya jamii za Kitanzania zimechambuliwa kwa kina | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kubaini maadili yaliyo-dumishwa na jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni | **Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kubainisha athari chanya na hasi za mfumo wa ukoloni katika maadili ya jamii za Kitanzania<br>**Kisamafunzo:** Elekeza wanafunzi kusikiliza kisamafunzo kuhusu maadili yaliyodumishwa na jamii mojawapo ya Kitanzania wakati wa ukoloni.<br>**Maswali na majibu:** Uliza maswali kuwezesha wanafunzi kueleza maadili yaliyodumishwa katika jamii nyingine za Kitanzania wakati wa ukoloni. | Maadili yaliyodumishwa na jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni yamebainishwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.3 Kuchambua jitihada za jamii za Kitanzania kupinga ukoloni na maadili ya kikoloni | (a) Kubaini sababu za jamii za Kitanzania kupinga uvamizi wa kikoloni, ukoloni na maadili yake | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini na kuorodhesha sababu za jamii za Kitanzania kupinga uvamizi wa kikoloni, ukoloni na maadili yake. **Maswali na majibu:** Uliza maswali kuwezesha wanafunzi kueleza sababu za jamii za Kitanzania kupinga uvamizi wa kikoloni, ukoloni na maadili yake. | Sababu za jamii za Kitanzania kupinga uvamizi wa kikoloni, ukoloni na maadili yake zimebainishwa | Picha kuonesha matendo ya kupinga ukoloni<br>Matini kuhusu harakati za jamii za Kitanzania kupinga ukoloni na maadili ya kikoloni | 18 |
| | | (b) Kujadili njia mbalimbali zilizotumika na jamii za Kitanzania kupinga uvamizi wa kikoloni, ukoloni na maadili yake | **Kisamafunzo:** Elekeza wanafunzi katika vikundi kusoma kisamafunzo na kuanisha njia mbalimbali zilizotumika na jamii za Kitanzania kupinga uvamizi wa kikoloni, ukoloni na maadili yake. | Njia mbalimbali zilizotumika na jamii za Kitanzania kupinga uvamizi wa kikoloni, ukoloni na maadili yake zimejadiliwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Majadiliano:** Ongoza vikundi kuwasilisha majibu yao darasani kwa majadiliano ya pamoja. | | | |
| | | (c) Kufafanua misingi na mbinu zilizotumika kupigania Uhuru wa Tanganyika na Zanzibar | **Mtaalamu mwalikwa:** Ongoza mtaalamu mwalikwa kuelezea misingi na mbinu zilizotumika kupigania uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.<br>**Majadiliano:** Ongoza vikundi vidogovidogo kujadili kisha kuwasilisha kwenye darasa kwa majadiliano ya pamoja. | Misingi na mbinu zilizotumika kupigania uhuru wa Tanganyika na Zanzibar imefafanuliwa kwa kina | | |
| | | (d) Kutathmini mchango wa harakati za kupinga uvamizi na | **Tafakuri:** Uliza maswali mbalimbali kupima mchango wa harakati za kupinga uvamizi na ukoloni | Mchango wa harakati za kupinga uvamizi na ukoloni katika kutunza maadili | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ukoloni katika kutunza maadili ya Kitanzania na kujenga uzalendo | katika kutunza maadili ya Kitanzania na kujenga uzalendo. | ya Kitanzania na kujenga uzalendo umetathiminiwa | | |
| 2.0 Kumudu historia ya ujenzi wa Taifa na maadili yake katika kipindi cha 1961-1966 | 2.1 Kuchambua mifumo ya uchumi, siasa, utamaduni, jamii na maadili iliyojengwa, 1961-1966 | (a) Kueleza hali ya uchumi, siasa, utamaduni, jamii na maadili mara baada ya uhuru | **Utafiti mdogo:** Elekeza kila mwanafunzi kusoma matini mbalimbali na kuandika maelezo kuhusu hali ya uchumi, siasa, utamaduni, jamii na maadili mara baada ya uhuru.<br>**Majadiliano:** Ongoza majadiliano ya vikundi kuhusu hali ya uchumi, siasa, utamaduni, jamii na maadili mara baada ya uhuru. | Hali ya uchumi, siasa, utamaduni, jamii na maadili mara baada ya uhuru imeelezwa | Matini kuhusu mifumo ya uchumi, siasa, utamaduni, jamii na maadili iliyojengwa 1961-1966 | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kutathmini mikakati na changamoto za ujenzi wa Taifa kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kijamii na kimaadili kipindi cha 1961-1966 | **Tafakuri:** Uliza maswali mbalimbali kupima mafaniko ya mikakati na changamoto za ujenzi wa Taifa kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kijamii na kimaadili kipindi cha 1961-1966. | Mikakati na changamoto za ujenzi wa Taifa kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kijamii na kimaadili kipindi cha 1961-1966 imetathiminiwa kwa kina | | |
| | 2.2 Kumudu historia ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar | (a) Kueleza chimbuko la Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini na kuandika maelezo kuhusu chimbuko la Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.<br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili na kuwasilisha kuhusu chimbuko la Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. | Chimbuko la Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar limeelezwa | Matini kuhusu Mapinduzi matukufu ya Zanzibar<br>Picha kuonesha watu walioshiriki katika Mapinduzi matukufu ya Zanzibar | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kubaini mchango wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar katika kujenga umoja, mshikamano na maadili miongoni mwa Wazanzibari | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini na kuandika maelezo kuhusu mchango wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar katika kujenga umoja, mshikamano na maadili.<br><br>**Maswali na majibu:** Uliza maswali kuhusu mchango wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar katika kujenga umoja, mshikamano na maadili miongoni mwa Wazanzibari. | Mchango wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar katika kujenga umoja na mshikamano miongoni mwa Wazanzibari umebainishwa | | |

## Kidato cha III

**Jedwali Na. 5:** *Maudhui ya Kidato cha III*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu historia ya ujenzi wa Taifa na maadili yake katika kipindi cha 1961-1966 | 1.1 Kumudu historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar | (a) Kufafanua chimbuko la Muungano wa Tanganyika na Zanzibar | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini kutoka vyanzo mbalimbali na kuandika maelezo kuhusu chimbuko Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. **Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili na kuwasilisha majibu yao. | Chimbuko la Muungano wa Tanganyika na Zanzibar limefafanuliwa kwa ufasaha | Matini kuhusu historia ya ujenzi wa Taifa na maadili 1961-1966<br>Kielelezo kuonesha muundo wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar | 16 |
| | | (b) Kueleza muundo na misingi ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini mbalimbali kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuchora | Muundo na misingi ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar imeelezwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | muundo na kuandika misingi ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.<br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili na kuwasilisha majibu yao. | | | |
| | | (c) Kutathimini Muungano wa Tanganyika na Zanzibar katika kujenga umoja na maadili ya Kitaifa | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini na kuandika maelezo kuhusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.<br>**Tafakuri:** Uliza maswali kuhusu mafaniko na changamoto zinazokabili Muungano wa Tanganyika na Zanzibar katika kujenga umoja na maadili ya Kitaifa. | Wanafunzi wametathmini Muungano wa Tanganyika na Zanzibar katika kujenga umoja na maadili ya Kitaifa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kutathmini ujenzi wa Taifa na maadili wakati wa Azimio la Arusha, 1967-1985 | 2.1 Kuchambua chimbuko la Azimio la Arusha na matokeo yake kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kimaadili | (a) Kujadili chimbuko la Azimio la Arusha | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini mbalimbali na kuandika maelezo kuhusu Azimio la Arusha.<br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili kuhusu chimbuko la Azimio la Arusha na kisha kuwasilisha kwa majadiliano ya pamoja. | Chimbuko la Azimio la Arusha limefafanuliwa kwa kina | | 16 |
| | | (b) Kufafanua misingi na mchango wa Azimio la Arusha katika ujenzi wa Taifa kiuchumi, kisiasa, kijamii na kimaadili | **Changanyakete:** Gawa wanafunzi katika vikundi vya maeneo ya uchumi, siasa, jamii na maadili na elekeza makundi katika eneo husika kusoma matini kuhusu Azimio la Arusha.<br>Elekeza kila kikundi kutoa mwakilishi kwenda kwenye | Misingi na mchango wa Azimio la Arusha katika ujenzi wa Taifa kiuchumi, kisiasa, kijamii na kimaadili umefafanuliwa kwa ufasaha | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | vikundi vingine kufundisha kuhusu misingi na mchango wa Azimio la Arusha katika ujenzi wa Taifa. | | | |
| | | (c) Kutathmini changamoto za Azimio la Arusha kiuchumi, kisiasa, kijamii na kimaadili | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini mbalimbali na kuandika maelezo kuhusu changamoto za Azimio la Arusha kiuchumi, kisiasa, kijamii na kimaadili. **Tafakuri:** Uliza maswali kuwezesha wanafunzi kutoa maoni yao kuhusu ukubwa wa changamoto za Azimio la Arusha kiuchumi, kisiasa na kijamii na kisha wapendekeze suluhisho kwa kila changamoto. | Changamoto za Azimio la Arusha kiuchumi, kisiasa, kijamii na kimaadili zimetathiminiwa kwa kina | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kueleza nafasi ya Tanzania katika kujenga uhusiano wa kikanda | (a) Kufafanua dhana ya uhusiano wa kikanda na ujenzi wa Taifa | **Mtaalamu mwalikwa:** Ongoza wanafunzi kusikiliza maelezo ya mtaalamu kuhusu uhusiano wa kikanda na ujenzi wa Taifa.<br>**Maswali na majibu:** Uliza maswali kuwezesha wanafunzi kueleza maana na umuhimu wa uhusiano wa kikanda na ujenzi wa Taifa. | Dhana ya uhusiano wa kikanda na ujenzi wa Taifa imefafanuliwa kwa ufasaha | Matini kuhusu nafasi ya Tanzania katika kujenga uhusiano wa kikanda | 16 |
| | | (b) Kueleza mchango wa Tanzania katika kukuza uhusiano wa kikanda na kujenga utaifa (EAC & SADC) | **Utafiti mdogo:**<br>Elekeza wanafunzi kusoma matini mbalimbali kuhusu mchango wa Tanzania katika kukuza uhusiano wa kikanda<br>**Mdahalo:** Gawa darasa katika makundi mawili, moja linalounga mkono kuwa Tanzania ina | Mchango wa Tanzania katika kukuza uhusiano wa kikanda na kujenga utaifa (EAC & SADC) umeelezwa kwa kina | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | mchango katika kukuza uhusiano wa kikanda na kujenga utaifa na lingine linalopinga kuwa hakuna mchango.<br>Simamia wanafunzi washiriki katika mdahalo ipasavyo. | | | |
| | | (c) Kubaini changamoto za uhusiano wa kikanda katika ujenzi wa Taifa | **Kisamafunzo:** Wasimulie wanafunzi kisa kuhusu changamoto ya uhusiano kati ya nchi moja na nyingine katika kanda mfano EAC na SADC.<br>**Maswali na majibu:** Uliza maswali kuhusu kisamafunzo ulichosimulia na kueleza changamoto nyingine za uhusiano wa kikanda katika ujenzi wa Taifa. | Changamoto za uhusiano wa kikanda katika ujenzi wa Taifa zimebainishwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. Kufanya kazi mradi ya historia ya Tanzania na maadili | 3.1 Kufanya kazi mradi ya historia ya Tanzania na maadili | Bainisha changamoto yoyote ya kihistoria iliyopo katika jamii, kisha andaa kazimradi ili kupata ufumbuzi. | ***Kazimradi***<br>Katika vikundi au mmoja mmoja, waongoze wanafunzi kubaini changamoto yoyote ya kihistoria au maadili katika jamii ya Tanzania, kisha waelekeze wanafunzi waandae mpango wa kutekeleza kazimradi hiyo | Changamoto ya historia au maadili imebainishwa, mpango wa kutekeleza kazi mradi umeandaliwa | Zana vifaa mbalimbali vinavyohusiana na kazimradi | 14 |

**Kidato cha IV**

**Jedwali Na. 6:** *Maudhui ya Kidato cha IV*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kutathmini historia ya Tanzania na maadili wakati wa uliberali, 1986 hadi sasa | 1.1 Kuchambua chimbuko la uliberali na utandawazi | (a) Kufafanua dhana ya uliberali na utandawazi | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini mbalimbali na kuandika maelezo kuhusu maana na viashiria vya uliberali na utandawazi.<br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili na kuandika maana na viashiria vya uliberali na utandawazi na kuwasilisha kwa ajili ya majadiliano ya pamoja. | Dhana ya uliberali na utandawazi imefafanuliwa kwa ufasaha | Matini kuhusu historia ya Tanzania na maadili wakati wa uliberali, 1986 hadi sasa<br>Matini kuhusu mfumo wa uliberali | 16 |
| | | (b) Kubaini vichocheo vilivyo-sababisha Tanzania kuingia katika mfumo wa uliberali na utandawazi | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma matini mbalimbali na kuorodhesha vichocheo vilivyosababisha Tanzania kuingia katika mfumo wa uliberali na utandawazi. | Vichocheo vilivyosababisha Tanzania kuingia katika mfumo wa uliberali na utandawazi vimebainishwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Mtaalamu mwalikwa:** Ongoza mtaalamu kuja kutoa maelezo kuhusu sababu zilivyosababisha Tanzania kuingia katika mfumo wa uliberali na utandawazi.<br>**Maswali na majibu:** Uliza maswali mbalimbali kuwezesha wanafunzi kufafanua vichocheo vilivyosababisha Tanzania kuingia katika mfumo wa uliberali na utandawazi. | | | |
| | | (c) Kueleza athari za uliberali na utandawazi katika mifumo ya uchumi, utamaduni, siasa na maadili | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi katika vikundi kufanya utafiti kwa kuuliza watu mbalimbali katika jamii wanamoishi kuhusu athari za uliberali na utandawazi katika mifumo ya uchumi, utamaduni, siasa na maadili. | Athari za uliberali na utandawazi katika mifumo ya uchumi, utamaduni, siasa na maadili imeelezwa kwa kina | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Matembezi ya galari:** Ongoza vikundi kubandika ripoti zao katika kuta za darasa na waambie wanafunzi kupita katika kila kundi na kusoma ripoti hizo. | | | |
| | | (d) Kubaini jitihada zinazohukuliwa na Tanzania kudhibiti athari mbaya za uliberali na utandawazi | **Fikiri-andika-jozisha-shirikisha:** Ongoza kila mwanafunzi kufikiri, kuandika na kushrikisha mwenzake mawazo yake na kisha katika kikundi kuhusu jitihada zinazochukuliwa na Tanzania kudhibiti athari mbaya za uliberali na utandawazi. | Jitihadi zinazochukuliwa na Tanzania kudhibiti athari mbaya za uliberali na utandawazi zimebainishwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kuishi maadili mema ya Kitanzania wakati wa uliberali na utandawazi | (a) Kujadili matendo ya uadilifu katika muktadha wa uliberali na utandawazi | **Tafakuri:** Uliza maswali kuhusu matendo ya uadilifu yanayopaswa kufanywa na wanajamii.<br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi kujadili na kuandika maelezo kuhusu matendo ya uadilifu katika muktadha wa uliberali na utandawazi. | Matendo ya uadilifu katika muktadha wa uliberali na utandawazi yamejadiliwa | Matini kuhusu maadili mema katika kipindi cha uliberali na utandawazi | 8 |
| | | (b) Kujadili mikakati mbalimbali ya kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu maadili ya Kitanzania | **Ziara ya mafunzo:** Ongoza wanafunzi kufanya ziara ya mafunzo katika taasisi za Serikali kama TAKUKURU, skauti na taasisi za dini na waulize mikakati mbalimbali waliyonayo kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu maadili ya Kitanzania. | Mikakati mbalimbali ya kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu maadili ya Kitanzania imebainishwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kumudu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 2.1 Kuchambua muundo wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | (a) Kuelezea muundo wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (sura kumi za katiba) | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi katika vikundi kufanya utafiti kwa kuuliza watu mbalimbali katika jamii wanamoishi kuhusu muundo wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi kujadili na kuandika maelezo kuhusu muundo wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Muundo wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (sura kumi za katiba) umeelezwa. | Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na matini mengine yanayohusu JMT. | 18 |
| | | (b) Kubainisha haki na wajibu wa raia kwa mujibu wa Katiba ya JMT | **Mtaalamu mwalikwa:** Ongoza mtaalamu kuja kutoa maelezo kuhusu haki na wajibu wa raia kwa mujibu wa Katiba ya JMT. | Haki na wajibu wa raia kwa mujibu wa Katiba ya JMT zimebainishwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Maswali na majibu:** Uliza maswali mbalimbali kuwezesha wanafunzi kufafanua haki na wajibu wa raia kwa mujibu wa Katiba ya JMT. | | | |
| | 2.2 Kuchambua misingi ya Katiba ya JMT | (a) Kueleza misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | **Kusoma Matini:** Kusoma matini kuhusu Katiba ya JMT. **Maswali na majibu:** Uliza maswali mbalimbali kuwezesha wanafunzi Kueleza misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeelezwa | Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na matini mengine yanayohusu JMT | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kubaini tunu za Taifa zilizotajwa katika Katiba ya JMT | **Maswali na majibu:** Uliza maswali mbalimbali kuwezesha wanafunzi kubaini tunu za Taifa zilizotajwa katika Katiba ya JMT.<br><br>**Wimbo:**<br>Ongoza wanafunzi kuimba wimbo wa Taifa na kubaini uhusiano uliopo kati ya katiba ya JMT na wimbo huo. | Tunu za Taifa zilizotajwa katika Katiba ya JMT zimebainishwa | | |
| | 2.3 Kutumia maarifa ya Katiba ya JMT katika shughuli mbalimbali za jamii na za kimaadili | (a) Kuelezea fursa za kiuchumi, kisiasa na kijamii zilizopo kwa mujibu wa Katiba ya JMT | **Kusoma Matini:**<br>Kusoma matini kuhusu fursa za kiuchumi, kisiasa na kijamii zilizopo kwa mujibu wa Katiba ya JMT.<br><br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi kujadili na kuandika maelezo kuhusu fursa za kiuchumi, kisiasa na kijamii zilizopo kwa mujibu wa Katiba ya JMT. | Fursa za kiuchumi, kisiasa na kijamii zilizopo kwa mujibu wa Katiba ya JMT zimeelezwa | Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na matini mengine yanayohusu JMT<br><br>Video, flash (kinyonyi) ya hotuba za viongozi mbalimbali wa kitaifa | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kueleza dhana ya ulinzi wa rasilimali za Taifa (ukuu wa nchi, wajibu wa raia, umuhimu wa ulinzi na athari za kutolinda rasilimali) | **Kusoma Matini:** Kusoma matini kuhusu dhana ya ulinzi wa rasilimali za Taifa (ukuu wa nchi, wajibu wa raia, umuhimu wa ulinzi na athari za kutolinda rasilimali).<br>**Maswali na majibu:** Uliza maswali mbalimbali kwa wanafunzi kuhusu dhana ya ulinzi wa rasilimali za Taifa (ukuu wa nchi, wajibu wa raia, umuhimu wa ulinzi na athari za kutolinda rasilimali). | Dhana ya ulinzi wa rasilimali za Taifa zimeelezwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 Kumudu muundo na kazi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 3.1 Kueleza muundo na kazi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | (a) Kuchambua muundo na kazi za mhimili tendaji (Executive) ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na matini nyingine kuhusu mhimili tendaji wa Serikali.<br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili kuhusu muundo na kazi za mhimili tendaji wa Serikali na kisha kuwasilisha kwa majadiliano ya pamoja. | Muundo na kazi za mhimili tendaji (executive) zimechambuliwa kwa kina | Matini kuhusu muundo na kazi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar<br>Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania | 17 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuchambua muundo na kazi za Bunge la Jamhuri na za Baraza la Wawakilishi Zanzibar | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na matini nyingine kuhusu mhimili wa Bunge la Jamhuri na Baraza la Wawakilishi.<br><br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili kuhusu muundo na kazi za Bunge la Jamhuri wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi kisha kuwasilisha<br><br>**Igizodhima:** Elekeza wanafunzi kuandaa na kuigiza kazi mbalimbali za Bunge la Jamhuri la Tanzania na Baraza la Wawakilishi. | Muundo na kazi za Bunge zimechambuliwa kwa kina | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuchambua muundo na kazi za Mahakama katika pande zote za Muungano | **Utafiti mdogo:** Elekeza wanafunzi kusoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na matini nyingine kuhusu mhimili wa Mahakama.<br><br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili kuhusu muundo na kazi za Mahakama na kisha kuwasilisha kwa majadiliano ya pamoja.<br><br>**Igizodhima:** Ongoza wanafunzi kuandaa na kuigiza kazi za Mahakama. | Muundo na kazi za Mahakama zimechambuliwa kwa kina | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kubaini muundo na kazi za Serikali za Mitaa | (a) Kueleza dhana na chimbuko la serikali za mitaa | **Fikiri-andika-jozisha-shirikisha:** Ongoza kila mwanafunzi kufikiri, kuandika, kumshirikisha mwezake na kisha kujadili katika kikundi kuhusu maana, umuhimu, sababu na uanzishwaji wa serikali za mitaa nchini.<br><br>**Mtaalamu mwalikwa:** Ongoza mtaalamu kueleza maana, umuhimu, sababu na uanzishwaji wa serikali za mitaa nchini.<br><br>**Maswali na majibu:** Uliza maswali mbalimbali kuwezesha wanafunzi kuandika muhtasari kuhusu maana, umuhimu, na chimbuko la serikali za mitaa nchini. | Dhana na chimbuko la serikali za mitaa limeelezwa kwa ufasaha | -Matini kuhusu muundo na kazi za serikali za mitaa<br><br>-Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania<br><br>-Sheria ya Serikali za Mitaa ya 1984 na mabadiliko yake | 11 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuchambua muundo na kazi za serikali za mitaa katika ngazi mbalimbali za Jamhuri ya Muungano | **Ziara ya mafunzo:** Ongoza wanafunzi kufanya ziara ya mafunzo katika ofisi ya serikali ya mtaa/kijiji kupata maelezo kuhusu muundo na kazi za serikali ya mtaa/kijiji.<br>**Majadiliano:** Ongoza wanafunzi katika vikundi kujadili kazi na kuchora muundo wa serikali ya mtaa/kijiji.<br>**Igizodhima:** Ongoza wanafunzi kuandaa na kuigiza kazi za serikali ya mtaaa/kijiji. | Muundo na kazi za mamlaka za miji na vijiji zimechambuliwa kwa ufasaha | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. Kufanya kazimradi ya historia ya Tanzania na maadili | 3.1 Kufanya kazimradi ya historia ya Tanzania na maadili | Kukamilisha na kuwasilisha taarifa ya kazimradi kuhusu historia ya Tanzania na maadili ulioianza kidato cha tatu | ***Kazimradi***<br>Ongoza wanafunzi kufanya kazi mradi katika mada zao kuhusu historia ya Tanzania na maadili (mwendelezo kutoka Kidato chaTatu).<br>Kisha, ongoza wanafunzi kuwasilisha kazi zao wakati wanaendelea kuandika ripoti zao za mwisho. | Utafiti kuhusu historia ya Tanzania na maadili umefanyika kikamilifu | Kompyuta, matini, vinasa sauti, Makala katika magazeti | 2 |

## Bibliografia

Abdul Sheriff and Ed Ferguson (eds.). (1991). *Zanzibar Under Colonial Rule*. James Currey.

Benjamin William Mkapa. (2019). *My Life, My Purpose: A Tanzanian President Remembers*. Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

Daniel K. Ndagala. (2018). *Utamaduni na Maendeleo Nchini Tanzania*.

Martin, H. Y. Kaniki (ed.). (1979). *Tanzania Under Colonial Rule*. Longman.

Isaria Kimambo and Anold Temu (eds.). (1969). *A History of Tanzania*. East African Publishing House.

Isaria Kimambo, Gregory Maddox and Salvatory Nyanto. (2017). *A New History of Tanzania*. Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

Issa Shivji, Saida Yahya Othman and Ng'wanza Kamata. (2020). *Development as Rebellion: A Biography of Julius Nyerere, Vol. 1-3*. Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

James Brennan. (2012). *Taifa: Making Nation and Race in Urban Tanzania*. Ohio University Press.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2022). *Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo*. Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

John Iliffe. (1979). *A Modern History of Tanganyika*. Cambridge University Press.

Julius Nyerere. (1967). *Freedom and Unity: a selection from writings and speeches, 1952-1965*. Oxford University Press.

Julius Nyerere. (1973). *Freedom and Socialism: a selection from writings and speeches, 1965-1967*. Oxford University.

MoEVT. (2014). In-Service Training Manual for Secondary Schools History Teachers. Secondary Education Department, MoEVT.

Wizara ya Utamaduni. (2022). *Sanaa na Michezo, Mwongozo wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania*.